Naungana na viongozi wa Kanisa la Waadventista wa Sabato na wazungumzaji wengine walionitangulia, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kibali chake cha kufanyika kwa kongamano la siku nne kuhusu uhuru wa kidini Afrika, linalohitimishwa hivi leo. Kwa niaba ya Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nakushukuru Mchungaji Mark Walwa Malekana, Mwenyekiti wa Kanisa la Waadventista wa Sabato Unioni ya Kaskazini mwa Tanzania na waumini wote wa Kanisa la Waadventista wa Sabato, kwa kumwalika Mheshimiwa Rais kuwa mgeni rasmi katika kufunga Kongamano hili muhimu. Licha ya kupokea na kuridhia mwaliko wenu, hakuweza kushiriki nanyi kutokana na majukumu mengi aliyonayo. Hivyo, amenituma kumwakilisha.

Napenda pia kuwapongeza kwa dhati viongozi wa Kanisa la Waadventista wa Sabato kutoka ndani na nje ya bara la Afrika na waumini wote wa dini mbalimbali mlioweza kushiriki Kongamano hili hapa Arusha. Kipekee, napenda kuushukuru uongozi wa Kanisa la Waadventista wa Sabato Tanzania na Chama cha Uhuru wa Kidini Barani Afrika, kwa maandalizi, uratibu na uwezeshaji wa Kongamano hili. Nimefahamishwa kwamba, katika siku hizi nne mmejadili kwa kina njia mbalimbali za kukuza uhuru na uvumilivu wa kidini kama msingi wa kuishi kwa amani, umoja na mshikamano miongoni wa jamii yenye imani mbalimbali za kidini.

1. **KUISHI PAMOJA KWA USALAMA NA UTULIVU BILA VURUGU AU VITA**

**Ndugu washiriki wa Kongamano na waumini;**
Nimejulishwa kwamba Kaulimbiu ya Kongamano hili ilikuwa: "Kuishi Pamoja kwa Amani Barani Afrika: Tunu Isiyopingika ya Dhamiri ya Binadamu" (*Peaceful Co-existence in Africa: The Undeniable Value of Human Conscience).* Kaulimbiu hii ni nzuri sana na ninawapongeza kwa uchaguzi wa dhima hii muhimu sana. Sababu yake ni kwamba amani ni tunu adhimu sana kwa Taifa lolote lile. Hakika, ipo mifano mingi inayotukumbusha kuwa kushindwa kuheshimu tofauti za kiimani kunaweza kuchochea vita na migogoro katika mataifa mbalimbali na kusababisha vurugu, vifo na hata kuathiri uchumi na maendeleo kwa ujumla. Baadhi ya migogoro inayojitokeza Barani Afrika, inatokana na imani kali za kidini. Taarifa zinaonesha kuwa, takriban nusu ya vifo vilivyohusishwa na ugaidi duniani vilitokea katika eneo la kati la Sahara (*Journey to extremism in Africa: Pathways to recruitment and Disengagement, 2023).* Vilevile, itikadi kali za kidini, zimeenea pia katika nchi nyingine za Bara la Afrika kama vile Nigeria, Msumbiji, Somalia na Sudani na kusababisha vifo, utekaji na watu kuyakimbia makazi yao.

**Ndugu washiriki wa Kongamano na waumini;**
Licha ya umuhimu mkubwa wa kuishi pamoja kwa amani, kiuhalisia siyo jambo rahisi *(not a simple endeavour)*. Ni lazima iwe juhudi endelevu *(it is a constant struggle)*. Amani inayosemwa katika Biblia, kitabu cha Nabii Isaya 11:6 kwamba *"Mbwamwitu ataishi pamoja na Mwanakondoo, Chui watapumzika pamoja na Mwanambuzi, Ndama na Simba watakula pamoja na mtoto mdogo atawaongoza"* siyo jambo rahisi hata kidogo! Napenda kuamini kwamba katika siku hizi 4 za kongamano mmejadili jambo hili kwa mapana yake na kwa kina. Bila shaka mmechambua namna au mbinu za kuwezesha watu wa imani tofuti tofauti za kidini kuishi pamoja kwa amani. Itoshe tu kusema kwamba, jambo muhimu ni kuheshimiana na kustahimiliana maana sote tumeumbwa na Mungu. Tuache kukashifu wenzetu kwa msingi kwamba imani yangu ni bora kuliko ya mwingine. Tutumie

zaidi saburi, mazungumzo *(inter-religious dialogue)*, na kualikana na kushirikiana katika shughuli mbalimbali za kijamii ili kujenga udugu, kuaminiana na kufikia maridhiano na amani.

**Ndugu washiriki wa Kongamano na waumini;**
Hata hivyo, mimi ninapoitazama Tanzania na Bara letu la Afrika, kwa ujumla ninaona kwamba changamoto ya kuishi pamoja kwa amani ina sura mbalimbali. Na hapa napenda ieleweke kuwa haya nitakayosema hayalengi dhehebu lolote la dini, ha hivyo naomba radhi kama itaonekana kuligusa dhehebu fulani. **Sura ya kwanza** ambayo tayari nimeielezea ni changamoto ya watu wa imani tofauti za kidini kuishi pamoja kwa amani. **Sura ya pili** ninayoiona ni ile ya watu wa imani moja ya kidini kushindwa kuishi pamoja kwa amani. Hapa naomba nifafanue kidogo. Siku hizi tunashuhudia magomvi na vurugu za aina mbalimbali miongoni mwa waumini wa imani moja, wakiwemo baadhi viongozi wa dini (Wachungaji au Mashekhe, Ma-Ustaadh, Wazee wa kanisa n.k.). Wote tunashuhudia viongozi wanaondoana au kufukuzana kwenye nyumba za ibada na hata kwenu ndugu zangu wa Kanisa la Waadventista wa Sabato ninaona nyaraka mbalimbali kwenye mitandao. Mfano ni za yule anayejulikana kama "Jicho la Mwewe" (sijui kama yupo nasi hapa uwanjani) ambazo zimejaa tuhuma nyingi, zinazojumuisha matumizi mabaya ya fedha na mali za kanisa, kugombea madaraka, kuajiriana kwa upendeleo, rushwa na kukosekana kwa haki kwenye chaguzi katika ngazi za *Union, Conference na Field.* Hata katika madhehebu mengine ya dini, mambo ni hayo hayo, japo kwa viwango tofauti tofauti. Nako kuna kuenguana kwenye uongozi, kuhamishwa kutoka kwenye mitaa, usharika, vigango, parokia au misikiti yenye sadaka kubwa na kupelekwa kwenye vituo vyenye maokoto kidogo! Ninashangazwa zaidi na kuwepo hata kwa tuhuma za ushirikina! Kwa maoni yangu, baadhi ya mambo haya yanatokana na kuwa baadhi ya viongozi wameigeuza dini kuwa ajira badala ya utumishi kwa Mungu. Wakati mwingine, tofauti miongoni mwetu zinatokana na tafsiri tofauti ya maandiko, kila mtu akijiona ndiye mwenye tafsiri sahihi.

**Ndugu washiriki wa Kongamano na waumini;**
Viongozi wetu wa dini mnayo nafasi na heshima ya pekee sana katika jamii yetu hapa Tanzania na nchi nyingine za Afrika, kama wawakilishi wa Mungu hapa duniani. Kwa unyenyekevu naomba nitoe rai kwenu watumishi wote wa Mungu, kutafakari mwenendo huu unaozidi kuota mizizi. Nafikiri jambo muhimu ni kudhibiti tamaa ya mali iliyopitiliza (magari, nyumba za kifahari, fedha n.k.) na uchu wa madaraka na kurudi kwenye wito wenu halisi. Tujinyenyekeshe kwa Mungu. Tena, naamini yafaa wote turudi kwenye utaratibu wetu mzuri wa kusemana na kuonyana kwa upendo au kindugu kanisani na misikitini ambao naona tunauacha na badala yake, tumehamia mitandaoni! Tusipofanya haya, kwa maoni yangu itakuwa vigumu sana kuhubiri na kujenga tunu ya kuishi pamoja kwa amani na wenzetu wa imani tofauti wakati sisi wenyewe wa imani moja tunashindwa kuishi pamoja kwa amani.

**Ndugu washiriki wa Kongamano na waumini;**

**Sura ya tatu** ni ile ya baadhi ya viongozi wa dini au dhehebu moja kujiambatanisha na chama kimojawapo cha siasa na kupelekea maoni yao binafsi ya kisiasa kutafsiriwa kwa ndiyo maoni ya dini au dhehebu wanaloliongoza. Katika hali kama hiyo, itakuwa vigumu kwa wafuasi wa vyama vingine vya siasa kuishi pamoja kwa usalama na utulivu na watu wa kile chama kingine chenye mrengo tofauti wa kisiasa. Hili ni jambo la hatari kwa umoja wa kitaifa. Aidha, hali kama hiyo inaleta changamoto kubwa katika uhusiano na mashirikiano baina ya Serikali ambayo haina dini na baadhi ya viongozi wa dini wenye mrengo dhahiri wa kisiasa. Wito wangu ni kutochanganya dini na siasa, kwa maana hiyo niliyoieleza.

**Ndugu washiriki wa Kongamano na waumini;**

**Sura ya nne** ni kwamba haitoshi tu kuishi pamoja kwa usalama na utulivu miongoni mwa watu wa imani tofauti na wale ambao tuna imani moja na mrengo tofauti wa kisiasa, bali pia kati yetu na viumbe wengine. Kwa maneno mengine, hatuna budi kuishi pamoja kwa amani na mazingira yetu *(peaceful co-existence with the environment)*. Changamoto ya uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi inazidi kukua na kuongezeka. Maandiko matakatifu yanatueleza kuwa hapo mwanzo, Mwenyezi Mungu aliumba kwanza dunia ikiwa na mazingira mazuri (bustani) kabla ya kumuumba mwanadamu, aliyemwagiza pamoja na mambo mengine kuitunza. Hata hivyo, kutokana na shughuli za kibinadamu, kumekuwepo uharibifu mkubwa wa mazingira duniani na kuongezeka kwa uzalishaji wa gesi joto kulikopelekea mabadiliko ya tabianchi, majanga ya ukame, mafuriko, maporomoko ya ardhi na kukauka kwa vyanzo vya maji. Kutokana na hali hiyo, tunashuhudia pamoja na mambo mengine, mizozo na migogoro mingi inayotokana na uhaba wa rasilimali maji. Hivyo, nawasihi Viongozi wa dini kuhimiza umuhimu wa kuishi katika hali ya usalama na amani na mazingira yetu kama njia mojawapo ya kudumisha uhuru kwa kidini kwa kuwa mazingira na rasilimali zake kama vile maji ni muhimu katika kumwabudu Mungu na kuwezesha sisi binadamu, wanyama, mimea, ndege na wadudu kuishi pamoja kwa amani na kwa kutegemeana.

**Sura ya tano** inahusu maadili mema katika jamii kama njia mojawapo ya kujenga jamii yenye amani na utulivu. Dini zina mchango mkubwa katika kujenga familia na jamii zenye maadili mema. Familia na jamii zinazozingatia mafundisho ya dini zinazingatia pia maadili mema na hivyo kupelekea jamii kuishi katika hali ya usalama na utulivu. Kinyume chake, palipo na mmomonyoko wa maadili vitendo viovu kama vile unyang'anyi, matumizi ya dawa za kulevya, ulevi wa pombe, uasherati, ubakaji, ulawiti na ushoga hushamiri. Hali kadhalika, matukio ya mauaji ya kikatili, ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto na wanawake, na ubadhirifu wa mali za umma. Hivyo, napenda kuwasihi viongozi wetu wa dini na washiriki wote wa kongamano, kusimamia kikamilifu suala la maadili mema katika jamii, kwa kuanzia kwetu sisi wazazi/walezi hadi kwa vijana na watoto wetu. Shauku yangu ni kuona jamii inayolinda, kutunza na kurithisha maadili mema kwa vizazi vijavyo na kukemea maovu kwa nguvu zote. Tunaweza kufikia azma hiyo endapo jamii yetu itakuwa na hofu ya Mungu.

**Ndugu washiriki wa Kongamano na waumini;**

Uhuru wa kidini tunaouona hivi sasa hapa nchini una misingi yake katika Katiba ya JMT na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na waasisi wa Taifa letu, pamoja na mambo mengine, kuhakikisha uhuru wa kidini wa watu wa dini zote. Nchi yetu ni miongoni mwa nchi zenye amani na utulivu katika Bara la Afrika. Kiini cha hali hii ni misingi iliyowekwa na waasisi wa Taifa letu iliyosisitiza umoja, mshikamano, kuheshimiana na kuondoa tofauti za kidini, kisiasa, rangi au kabila. Kama hiyo haitoshi, uhuru wa kidini hapa nchini unatambuliwa na kulindwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika Ibara ya 19 (1) ***"Kila mtu anastahili kuwa na uhuru wa mawazo, imani na uchaguzi katika mambo ya dini, pamoja na uhuru wa mtu kubadilisha dini au imani yake."*** Ibara hii inatoa haki kwa kila mtu kuchagua imani anayoitaka na hata kubadili dini kwa hiari yake. Katika kulinda uhuru wa kidini nchini, Katiba katika ibara ya 19 (2), pamoja na mambo mengine, imezifanya shughuli za uendeshaji wa jumuiya za dini kuwa nje ya shughuli za mamlaka ya nchi, nanukuu ***"Kazi ya kutangaza dini, kufanya ibada na kueneza dini itakuwa huru na jambo la hiari la mtu binafsi, na shughuli na uendeshaji wa jumuiya za dini zitakuwa nje ya shughuli za za mamlaka ya nchi."*** Katika muktadha huo, Serikali inashirikiana kwa karibu na viongozi wa dini zote nchini hasa katika sekta za afya na elimu na kushauriana kutatua changamoto mbalimbali zinazojitokeza na kuhakikisha shughuli za dini zinaendeshwa kwa amani na utulivu hapa nchini. Hali kadhalika, ibara ya 19 (3) inataka shughuli za uenezaji dini, kufuata sheria za nchi, nanukuu ***"Hifadhi ya haki zilizotajwa katika ibara hii itakuwa chini ya taratibu zilizowekwa na sheria ambazo ni muhimu katika jamii ya kidemokrasia kwa ajili ya usalama wa jamii, amani katika jamii, maadili ya jamii na umoja wa kitaifa".***

**Ndugu washiriki wa Kongamano na waumini;**

Sambamba na misingi ya kuishi pamoja kwa amani iliyowekwa katika Katiba, nchi yetu ina mfano mzuri wa namna ya kukabiliana na kuvunjika kwa amani miongoni mwa jamii kutokana na tofauti za kidini. Kubwa, ni uwepo wa chombo kinachojulikana kama Kamati ya Maridhiano na Amani chenye wajumbe kutoka madhehebu yote ya kidini. Kamati hii ipo katika ngazi ya taifa, mkoa na wilaya na imejiwekea utaratibu wa kukutana mara kwa mara ili kujenga udugu, kushauriana na kuelimishana juu ya maeneo yenye kuleta kuhitilafiana ili kujenga hali ya kuaminiana na kushirikiana. Aidha, kamati hii, licha ya kualikana kwenye shughuli za dhehebu moja moja, zipo pia shughuli za mashirikiano ya pamoja kama vile michezo. Serikali pia huwaalika viongozi wa kamati hiyo kwenye shughuli mbalimbali za kitaifa. Mchango wa Kamati hii tunauona katika kuhimiza na kudumisha umoja, maridhiano na utulivu nchini, kukemea maovu na kuhimiza mafundisho sahihi ya kidini yanayojenga uwezo wa kustahimili, kuvumiliana na kuheshimiana katika imani zetu na kuepuka mafundisho ya chuki kwenye nyumba za ibada au kupitia mitandao ya kijamii na mihadhara.

## 2. HITIMISHO

Ninapoelekea kuhitimisha, napenda kusisitiza kuwa kukosekana kwa elimu ya kutosha kuhusu dini na ustahimilivu wa kidini, kukosa/kunyimwa haki, miiko/desturi ambazo ni vikwazo kwa wanadamu wengine, pamoja na umaskini na ufukara, vimekuwa vyanzo vya

kuvuruga hali ya usalama na utulivu. Aidha, napenda kuwahakikishia kuwa Serikali imepokea na itazifanyia kazi changamoto zilizoelezwa hapa ikiwemo usaili na mitihani kufanyika siku ya sabato. Baadhi ya changamoto hizi zinahitaji mashauriano na wadau mbalimbali na siyo uamuzi wa Serikali peke yake.

Mwisho kabisa, nawakumbusha kuhusu uchaguzi wa Serikali za Mitaa hapa Tanzania, unaotarajiwa kufanyika tarehe 27 Novemba mwaka huu. Ninawaomba Viongozi wa dini na waamini wote kuendelea kuombea uchaguzi huu ili ufanyike katika hali ya amani na utulivu. Aidha, nawapongeza tena waandaaji wa Kongamano hili la Uhuru wa Kidini ambalo linafikia ukomo hivi leo. Ni matumaini yangu kuwa, limekuwa ni jukwaa zuri lililotuwezesha kujadili masuala muhimu yahusuyo uhuru wa kidini na kuishi pamoja kwa amani na kwamba sasa mko tayari kwenda kutekeleza mapendekezo mliyokubaliana kwa kuzingatia mazingira mahsusi ya kila nchi ili kuimarisha amani na usalama katika nchi zetu za bara la Afrika.

Baada ya kusema hayo, sasa ninayo heshima kutamka kwa niaba ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa Kongamano la nne la Uhuru wa Kidini katika Bara la Afrika limefungwa rasmi.

***Sabato Njema...(Njema sana na hasa ya leo)***

***Makambi 2024....(Nitakwenda na familia yangu)***